# CHUO KIKUU CHA MTAKATIFU AGUSTINO CHA TANZANIA

**S.L.P 307 MWANZA, TANZANIA**

**Simu:** 028 29 81186/7
**Nukushi:** 028 29 81185

**Barua pepe:** sautmalimbe@saut.ac.tz
**Tovuti:** www.saut.ac.tz


## TAARIFA KWA UMMA

KUTOONEKANA KWA MFANYAKAZI WA CHUO, **PADRE CAMILUS NIKATA**

Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania (SAUT) kimepokea kwa mshtuko mkubwa taarifa iliyotolewa na Baba Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Songea, Mhashamu Askofu Damian Dallu kuhusu kutoonekana kwa Padre Camilus Nikata ambaye ni padre wa jimbo lake na taarifa hii kuenea kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii tangu siku ya Jumatano tarehe 8 Oktoba 2025.

Kwa namna ya kipekee Uongozi wa SAUT unapenda kuuhabarisha Umma kuwa Padre Camilus Nikata ni Mhadhiri wetu katika Idara ya Mawasiliano ya Umma na alikwenda Dodoma kwenye mafundisho ya moyo ya mapadre wanaofundisha katika vyuo vikuu vya kikatoliki nchini vilivyo chini ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) kama ilivyoeleza taarifa ya Baba Askofu Mkuu Damian Dallu.

Ofisi ya Baba Askofu Mkuu ilichukuwa jukumu la kulitaarifu jeshi la polisi kwa ajili ya uchunguzi baada ya juhudi zote za kumtafuta kufanyika bila ya mafanikio.

Kufuatia tukio hili la kutoonekana kwa Mhadhiri wetu, Chuo kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania (SAUT) kupitia ofisi ya Chaplaincy imeandaa sala maalum kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu kumkinga na maovu yote, kumwimarishia ulinzi na kumwongezea usalama Padre Nikata.

**Imetolewa na**
**Ofisi ya Uhusiano na Mawasiliano - SAUT**
**13 Octoba 2025**